# CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA

## TAARIFA YA MHESHIMIWA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA KWA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE KUHUSU UJENZI WA JENGO LA VIPIMO NA VIWANGO AWAMU YA KWANZA – CBE DAR ES SALAAM

**TAREHE 10 MACHI, 2026**

## 1.0 Utangulizi

### 1.1 Kuanzishwa kwa Taasisi

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 31 ya mwaka 1965 kama taasisi ya Serikali yenye mamlaka ya kisheria. Lengo kuu la kuanzishwa kwake ni kutoa elimu ya biashara, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu. Chuo kilizinduliwa rasmi Januari 1965 na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

CBE ipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, aidha Chuo hiki kina kampasi nne zilizoko katika Mikoa ya: Dar es Salaam (Makao Makuu), Dodoma, Mwanza, na Mbeya.

### 1.2 Dira ya Chuo

Kuwa Chuo kinachoongoza kwa kutoa elimu yenye kuleta mabadiliko chanya yenye kujenga uwezo wa kibiashara.

### 1.3 Dhima ya Chuo

Kutoa elimu yenye kukidhi mahitaji ya jamii kwa stadi za biashara, na kutoa huduma bora kwa jamii kwa kupitia tafiti na ushauri wa kitaalamu.

## 2.0 Majukumu Ya Taasisi

Majukumu ya Chuo cha Elimu ya Biashara yapo kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 31 ya mwaka 1965 pamoja na kanuni zake, majukumu hayo ni pamoja na:

i) Kutoa mafunzo ya elimu katika fani za biashara;
ii) Kufanya tafiti katika fani za biashara; na
iii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika fani za biashara.

## 3.0 Muundo Wa Utawala Wa Taasisi

### 3.1 Uongozi wa Chuo

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kinaendeshwa chini ya mfumo wa utawala ulio wazi na uliopangwa vizuri. Chombo cha juu cha maamuzi ni Bodi ya Uongozi wa Chuo, inayoundwa na Mwenyekiti, Mkuu wa Chuo (Katibu), pamoja na wajumbe wengine sita (6). Mkuu wa Chuo, ambaye anasimamia shughuli za kila siku, husaidiwa na manaibu wawili: Naibu Mkuu wa Chuo anayeshughulika na Masuala ya Taaluma, Utafiti na Ushauri wa kitaalam (DR-ARC) na Naibu Mkuu wa Chuo anayehusika na Mipango, Fedha na Utawala (DR-PFA).

### 3.2 Idadi ya Watumishi na Maendeleo ya Watumishi

Idadi ya watumishi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) imeendelea kuongezeka na kufikia watumishi **511** kwa takwimu za Desemba 2025. Kati ya hao, 495 ni wa kudumu na 16 ni wa mikataba. Watumishi wa kitaaluma ni 254 (49.7%) na wa uendeshaji/utawala ni 257 (50.3%). Kwa mtazamo wa jinsia, wanawake ni 203 (39.7%) na wanaume 308 (60.3%).

Kati ya watumishi wanataaluma, 7 ni Maprofesa, 58 wana shahada za uzamivu (PhD), 168 wana shahada za uzamili (Masters degree) na 22 wana shahada ya kwanza (Bachelor degree). Miongoni mwa watumishi hawa wamesoma katika vyuo vya Tanzania na vya kimataifa kama:- Freiburg University (Germany), TWTH Aachen University (Germany), Melbourne University (Australia), KwaZulu-Natal University (South Africa), Alberta University (Canada), Stockholm University (Sweden), Dalian University and Dangobei University (China), University of Eastern Finland (Finland), Southwestern University of Finance and Economics (China), Saint Petersburg State University (Russia), Andhra University and Kerala University (India).

Chuo kimeendelea kufanya jitihada za kupambana na upungufu wa rasilimali watu, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Chuo cha Elimu ya Biashara kilipata kibali cha kuajiri watumishi **24** ambao kufikia Desemba 2025 watumishi 4 walikuwa tayari wameripoti kazini.

Kwa kuongezea, kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 CBE imefanikiwa kupata kibali cha kuajiri nafasi **57** ambapo nafasi 30 ni kwa ajili ya watumishi wa kitaaluma na 27 kwa watumishi waendeshaji.

#### 3.2.1 Maendeleo katika Rasilimali Watu

Hadi Desemba 2025, jumla ya watumishi **91** wapo katika masomo ya muda mrefu; kati yao 72 ni wa kitaaluma na **19** ni wa uendeshaji/utawala. Watumishi **67** wanadhaminiwa na Chuo, huku **24** wakiwa na vyanzo vingine vya ufadhili.

## 4.0 Mafanikio katika Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi

### 4.1 Utekelezaji wa Majukumu ya CBE kwa Miaka Mitano, 2020 – 2025


Kwa kipindi cha miaka mitano, CBE imefanya maendeleo makubwa katika maeneo ya taaluma, utafiti na ushauri wa kitaalam. Kwa ujumla, maeneo haya matatu yamechangia kuimarisha taswira ya chuo, kuongeza mapato, kuibua maarifa mapya, na kupanua mchango wa CBE kitaifa na kimataifa.

### 4.2 Taaluma

Katika kipindi cha miaka mitano, Chuo cha Elimu ya Biashara kimepata mafanikio makubwa na ya kuridhisha ikihusisha, kutoa mafunzo ya elimu katika fani za biashara, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika fani za biashara, kufanya maendeleo ya miundombinu ya kujifunzia na kufundishia.

#### 4.2.1 Ongezeko la Udahili wa Wanafunzi, Mitaala na Programu

Katika kipindi cha miaka mitano (2021/2022 – 2024/2025), idadi ya wanafunzi walioandikishwa imeongezeka kutoka wanafunzi **12,987** hadi kufikia wanafunzi **24,957**, sawa na ongezeko la wanafunzi **11,970 (**takribani **92.2%).** Ukuaji wa idadi ya wanafunzi umeoneshwa katika mchoro namba 1.




Ongezeko hili linaonesha mwitikio mkubwa wa jamii kwa programu za CBE pamoja na utekelezaji wa sera ya elimu bila ada unaoendelea chini ya Serikali ya Awamu ya Sita.

### 4.2.2 Idadi ya Mitaala

Katika kipindi cha miaka mitano, Chuo kimeendelea kupanua na kuboresha mitaala ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya teknolojia. Hadi kufikia Juni 2025, CBE ilikuwa na mitaala **63** iliyopitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET). Katika kipindi cha Julai-2025 - Februari 2026, mitaala mipya 8 imepata ithibati, hivyo kufanya jumla ya mitaala iliyopitishwa kufikia **71.** Aidha, mitaala mingine 28 ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji/uthibitishaji. Mitaala mipya iliyopata ithibati katika kipindi cha Julai-Desemba 2025 ni: -

a) Bachelor of Banking & Credit Management with Apprenticeship (NTA Level 7-8),
b) Bachelor of Digital Technologies Solution Management with Apprenticeship (NTA 7-8),
c) Bachelor of Degree in Business Administration – Double Degree (NTA 7-8),
d) Bachelor of Digital Marketing (NTA 7-8),

e) Bachelor of Accountancy and Economics with Education (NTA 7-8),
f) Bachelor of Commerce and Accountancy with Education (NTA 7-8),
g) Masters of Marketing and Public Relations- (NTA Level 9), na
h) Master of Business Administration in Leadership and Governance (MBA – Leadership & Governance).

#### 4.2.3 Programu za Uanagenzi

CBE imeboresha mitaala yake ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya teknolojia, ikisisitiza elimu yenye ujuzi wa vitendo. Kupitia Programu ya Uanagenzi, wanafunzi watatumia nusu ya muda darasani na nusu kazini ili kupata uzoefu halisi wa kazi. NACTVET imeridhia mtaala mpya wa **Bachelor of Digital Technologies Solutions Management with Apprenticeship** unaotekelezwa kwa ushirikiano wa CBE na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-Government Authority (eGA)). Vilevile, mtaala wa **Bachelor of Banking & Credit Management with Apprenticeship** utatekelezwa kwa ushirikiano wa CBE na Benki ya Finca. Pia, makubaliano yamesainiwa na WMA, TBS, na Equity Bank kwa ajili ya programu za Uanagenzi katika fani husika.

#### 4.2.4 Program Atamizi za Biashara (Incubation)

Mpango wa Atamizi za Biashara ulioanzishwa mwaka wa masomo 2021/2022 umeendelea kuendeleza ubunifu na ujasiriamali kwa vijana. Hadi Desemba 2025, jumla ya vijana/bunifu 773 wamesajiliwa katika atamizi za biashara na teknolojia za Chuo. Kati yao, 278 (36%) wapo hatua ya maandalizi (Pre-incubation), 75 (9.7%) wapo hatua ya atamizi (Incubation) na 420 (54.3%) wapo hatua ya baada ya atamizi (post-incubation). Mpango huu unalenga kutoa mazingira bora ya kukuza bunifu, kuwajengea vijana uwezo wa kiutendaji na kuwaunganisha na fursa za soko, mitaji na ushauri wa kitaalamu.

#### 4.2.5 Umataifishaji / Mashirikiano

Chuo kimeendelea kupanua ushirikiano wa kitaifa na kimataifa katika kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa suluhisho za kibiashara kwa jamii. Kitaifa, hadi February 2025 CBE ilikuwa na washirika 18 (taasisi za umma 9 na sekta binafsi 9). Taasisi za umma zinajumuisha

SIDO, TBS, WMA, LATRA, TCCIA, MUHAS, WRRB, BRELA na eGA. Taasisi binafsi ni TCDC, CEO roundtable, EACB, Malembo farm, AFM, JR institute of Technology na Benki ya Equity, Benki ya FINCA. Kimataifa, Chuo kina ushirikiano na vyuo vikuu na taasisi saba nje ya nchi ambazo ni University of Eastern Finland (Finland), South Western University of Finance and Economics - SWUFE na Sichuan Vocational College Of Finance And Economics (China), Suleyman Demirel University (Uturuki), Friedrich-Alexander-Universität Erlangen-Nürnberg (Ujerumani), Wolkite University (Ethiopia) na University of Western Cape (Afrika ya Kusini); ushirikiano huu unawezesha kubadilishana wahadhiri/wanafunzi, masomo ya Uzamili na Uzamivu, na tafiti za pamoja.

Vilevile, Chuo kimeanzisha programu ya shahada mbili (Double Degree) kwa ushirikiano na SWUFE ambapo wanafunzi 17 wamekwishadahiliwa; wanafunzi hawa watasoma sehemu ya masomo yao CBE na sehemu nchini China na hatimaye kutunukiwa shahada mbili, hivyo kuongeza ubobezi wao wa kimataifa na ushindani kwenye soko la ajira.

## 4.3 Tafiti


### 4.3.1 Miradi ya Tafiti

Katika kipindi cha miaka mitano (2020 - 2025), CBE imefanikiwa kupata ufadhili wa miradi mbalimbali ya utafiti ikijumuisha **miradi ya tafiti tisa** iliyofadhiliwa na taasisi kama Umoja wa Ulaya (EU), Codesria, the Swedish Programme for ICT in Developing Regions (SPIDER), Academy of Finland, VW Foundation, Research Council of Finland, German Federal Ministry of Food and Agriculture, Finland Ministry of Foreign Affairs, COSTECH na Tanganyika Christian Refugee Services (TCRS). Jumla ya **miradi sita ya utafiti** inaendelea kwa mwaka huu wa fedha (2025/2026).

Aidha, Chuo hutenga bajeti kupitia mapato ya ndani kila mwaka kwa ajili ya shughuli za utafiti, ambapo imeonekana ongezeko la bajeti kutoka TZS 46 milioni (2018/2019) hadi TZS 350 milioni (2023/2024). Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Chuo kimetenga TZS 350 milioni kwa ajili ya tafiti za ndani ambapo tafiti saba (7) zinaendelea Februari 2026.

### 4.3.2 Machapisho

Kwa upande wa machapisho, katika kipindi cha miaka mitano, Chuo kimefanikiwa kufanya jumla ya machapisho **437** kwenye majarida ya kimataifa na kitaifa, kutoka **70 (2021) hadi 437 (2025)**. Aidha kwa mwaka huu wa fedha, Julai-Desemba 2025 pekee, machapisho 148 yameshafanyika. Takwimu hizi katika mchoro namba 2 zinaonesha ukuaji mzuri wa machapisho unaodhihirisha mchango wa chuo katika kuongeza uelewa na kutatua matatizo ya kijamii.




Aidha, ubora wa machapisho haya unajidhihirisha kwani mengi yamechapichwa katika majarida yenye hadhi kubwa kimataifa / yaliyo katika "*indexing databases*" zinazoaminika kimataifa. Jedwali namba moja linaonesha idadi ya machapisho ya robo ya pili ya mwaka huu 2025/2026 kwenye "*indexing databases*" mbalimbali zinazoaminiwa kimataifa.

**Jedwali Na. 1: Ubora wa Machapisho (2025 - 2026)**

| ***Indexing Database*** | **Idadi ya Machapisho** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Scopus / Web of Science | 11 | 31% |
| DOAJ | 8 | 23% |
| EBSCO | 6 | 17% |
| AJOL | 6 | 17% |
| IEEE | 2 | 6% |
| ProQuest | 1 | 3% |

| | | |
|---|---|---|
| Other | 1 | 3% |
| **TOTAL** | **35** | **100%** |

Kufikia Desemba 2025, idadi ya nukuu (citations) kwenye Google Scholar ilifikia 15,482 ikilinganishwa na 14,218 zilizorekodiwa Desemba 2024. Kuongezeka kwa nukuu (citations) kunaonesha kuwa tafiti za chuo zinaonekana zaidi, zinaaminika, na zina athari kubwa katika jamii ya kitaaluma, hali inayochangia kuongeza sifa ya chuo, nafasi yake katika viwango vya vyuo duniani, pamoja na fursa za ushirikiano na ufadhili wa utafiti.


Ili kuyafanya machapisho haya yawafikie watu wengi na yaweze kufikia lengo la kutatua changamoto mbalimbali za kijamii, chuo kimeanzisha kanzidata (Repository) ambayo machapisho 729 ya wanataaluma na tasnifu (*theses and dissertations)* za wanafunzi zote huwekwa na kufikiwa na watu kirahisi kupitia kiungo hiki cha tovuti. https://dspace.cbe.ac.tz/home.

Chuo pia kina **Jarida la Elimu ya Biashara (The Business Education Journal – BEJ)** ni jarida la kitaaluma linalopitia makala kwa mfumo wa uhakiki wa wataalamu (peer-reviewed) linalochapishwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (College of Business Education – CBE), na hadi sasa lina jumla ya **machapisho 140**. BEJ ni jukwaa la uchapishaji wa taaluma mbalimbali lenye lengo la kuendeleza na kukuza taaluma ya biashara na usimamizi kwa kuchapisha tafiti bunifu na zenye mchango mkubwa kwa wanataaluma, viongozi, na wasimamizi wa kitaaluma duniani kote (https://bej.cbe.ac.tz/index.php/bej).

### 4.3.3 Kongamano


Chuo kimeendelea kuandaa Kongamano la Maendeleo ya Biashara na Uchumi (Business and Economic Development Conference - BEDC) ambapo BEDC ya sita (6) ilifanyika tarehe 12–13 Novemba 2025, Mtumba - Dodoma na kupokea jumla ya tafiti **101**. BEDC 2026 imepangwa kufanyika tarehe 6 – 7 Oktoba 2026. Tafiti zilizowasilishwa kwenye makongamano kwa kipindi cha miaka 6 ni **545** kama inavyoonekana katika mchoro namba 3. Kama mchoro unavyoonesha, kiujumla idadi ya mawasilisho kwenye makongamano

yamekuwa yakiongezeka kulinganisha na idadi ya mwanzo. Hii inaonesha kuwa chuo kinafanya juhudi kubwa kuisaidia jamii kupitia mawasilisho ya wanataaluma kwenye makongamano haya.




### 4.3.4 Nafasi ya Chuo Kitaifa na Kimataifa

Kwa miaka mitatu mfululizo, Chuo kimeshika nafasi kati ya **7** na **8** kati ya **47** katika ubora wa elimu katika Vyuo vya Elimu ya juu hapa nchini. Hii ni kama inavtoonekana kwenye mchoro namba 4.




Ubora huu wa Chuo unatokana na vigezo mbalimbali vinavyotumika kupima ubora wa vyuo hapa duniani vikiwemo viwango vya elimu ya Wahadhiri, ubora machapisho wanayochapisha wanataaluma, idadi ya tafiti zinazofanywa na wanataaluma pamoja na vigezo vingine. Nafasi


hii ya 8 ni kielelezo tosha kuwa Chuo kinajitahidi kufanya kazi kwa bidii ili kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, Sera na Miongozo mbalimbali iliyowekwa, tunakuahidi tutaendeleza juhudi hizi na chuo kitaendelea kufanya vizuri zaidi.

### 4.4 Ushauri wa Kitaalamu

Katika kipindi cha miaka mitano, Chuo cha Elimu ya Biashara kimefanya mambo mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake mama ya Ushauri wa Kitaalam.

#### 4.4.1 Mafunzo ya Ujasiriamali

Katika kutekeleza ajenda ya Serikali ya kukuza ujasiriamali, CBE imekuwa ikitoa mafunzo ya ujasiriamali bila ada kwa wajasiriamali wadogo, wanawake na vijana katika kampasi zake. Kwa kipindi cha miaka mitano, jumla ya wajasiriamali **4,500** walipatiwa mafunzo hayo. Mchoro namba 5 unaonesha ukuaji wa idadi ya wajasiriamali waliopokea mafunzo kwa miaka mitano.




Aidha, kwa mwezi wa Desemba 2025 pekee, Chuo kilitoa mafunzo kwa wajasiriamali **1,240** katika Kampasi za Mwanza (440) na Mbeya (800). Katika mwezi huu wa Machi 2026 mafunzo haya yatatolewa katika Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma ambapo takribani wanufaika **1,500** watafikiwa.

Ongezeko hili linaashiria kuwa chuo kinaendelea kupanua programu za mafunzo ya ujasiriamali na kuwafikia washiriki wengi zaidi kila mwaka, hivyo kuchangia maendeleo ya ujuzi wa biashara na kujiajiri katika jamii.

### 4.4.2 Mafunzo kwa Wahudumu wa Mabasi na Madalali wa Mali za Kudumu

Chuo cha Elimu ya Biashara kimeendelea kuendesha mafunzo kwa makundi maalum, yakiwemo wahudumu wa mabasi na mawakala wa mali zisizohamishika, ili kuongeza ufanisi na kuimarisha urasimishaji wa shughuli zao. Tangu mafunzo haya yaanze mwaka 2023 Chuo kimewafundisha jumla ya wahudumu wa mabasi 2,418 na mawakala wa mali zisizohamishika 45 katika kampasi za Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya (Jedwali Na. 2). Aidha, katika kipindi cha Julai-Desemba 2025, mafunzo haya yaliendelea na kuwafikia washiriki 2418 wa wahudumu wa mabasi; makusanyo yalifikia **TZS 483,600,000** na **TZS 96,720,000** (sawa na 20%) ziliwasilishwa kwa Chuo kama mapato (Jedwali Na. 3).

**Jedwali Na. 2: Mafunzo ya Wahudumu wa Mabasi na Madalali wa Mali za Kudumu**

| **Kundi la Mafunzo** | **Kampasi** | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Dar es Salaam** | **Dodoma** | **Mwanza** | **Mbeya** | |
| Wahudumu wa Mabasi (Bus Crew Attendants) | 452 | 412 | 832 | 722 | **2,418** |
| Wakala wa Mali Isiyohamishika (Real Estate Agents) | 45 | - | - | - | **45** |

**Jedwali Na. 3: Mapato yatokanayo na Mafunzo ya Wahudumu wa Mabasi (Julai - Desemba 2025)**


| **KAMPASI** | **WASHIRIKI** | **ADA (TZS)** | **MAKUSANYO (TZS)** | **MAPATO KWA CHUO (20%) (TZS)** |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 412 | 200,000 | 82,400,000 | 16,480,000 |
| Dar es Salaam | 452 | 200,000 | 90,400,000 | 18,080,000 |
| Mwanza | 832 | 200,000 | 166,400,000 | 33,280,000 |
| Mbeya | 722 | 200,000 | 144,400,000 | 28,880,000 |
| **Jumla** | **2,418** | **200,000** | **483,600,000** | **96,720,000** |

Takwimu hizi zinaonesha mchango wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa jamii kupitia utoaji wa mafunzo kwa makundi maalum kama wahudumu wa mabasi na mawakala wa mali

zisizohamishika. Kupitia mafunzo haya, Chuo kinasaidia kuongeza ujuzi, ufanisi na urasimishaji wa shughuli zao za kiuchumi. Hatua hii pia inachangia kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii pamoja na kukuza taaluma na maadili katika sekta husika.

### 4.4.3 Huduma za Ushauri wa Kitaalamu


Katika kipindi cha miaka mitano (2020-2025), Chuo kilitekeleza jumla ya miradi 25 ya ushauri wa kitaalamu. Miradi hii ilifanywa kwa taasisi mbalimbali kama: - Stockholm University, TBS, Air Tanzania, TenMet, TAMISEMI, VFRESH, UPLC n.k. Idadi ya miradi kwa kipindi cha miaka mitano ni kama inavyoonekana kwenye mchoro namba 6. Aidha, katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2025/2026 (Oktoba–Desemba 2025), Chuo kinaendelea na mradi mmoja (1) wenye thamani ya TZS 87,600,000 toka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) huku maombi ya kazi za ushauri wa kitaalamu manne (4) yakiwa kwenye hatua za tathmini/maamuzi.




Kama inavyoonekana kwenye mchoro namba 6 mwenendo wa ushauri wa kitaalamu uliotolewa na Chuo katika kipindi cha miaka ya masomo 2020/2021 hadi 2024/2025. Idadi ya shughuli za ushauri iliongezeka kutoka 2 mwaka 2020/2021 hadi kufikia 8 mwaka 2022/2023, ikionyesha kuimarika kwa ushiriki wa Chuo katika kutoa utaalamu kwa wadau mbalimbali. Ingawa kulikuwa na kupungua hadi 4 mwaka 2023/2024 na 2024/2025, kiwango hiki bado kinaonesha mchango wa Chuo kwa jamii kupitia utoaji wa ushauri wa kitaalamu

unaosaidia taasisi, biashara na jamii kwa ujumla kuboresha utendaji na kufanya maamuzi yenye tija.

Pia kwa kipindi hiki, chuo kimetoa kozi **107** za mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali za biashara (Mchoro namba 7)




Mchoro namba 7 unaonesha mwenendo wa mafunzo ya muda mfupi yaliyotolewa na Chuo kati ya mwaka wa masomo 2020/2021 hadi 2024/2025. Idadi ya mafunzo imeongezeka kutoka 17 mwaka 2020/2021 hadi kufikia kilele cha 32 mwaka 2023/2024, kabla ya kushuka kidogo hadi 20 mwaka 2024/2025. Hali hii inaonesha juhudi za Chuo katika kutoa mafunzo ya kujenga ujuzi kwa wadau na jamii, hivyo kuchangia maendeleo ya rasilimali watu na kuboresha ufanisi katika sekta mbalimbali.

## 5.0 Maendeleo katika Miundo mbinu ya Kujifunzia

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kinandelea na miradi mbalimbali ya ujenzi na kufanya uboreshaji wa Miundombinu yake ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kutoa elimu bora, kukuza biashara na uchumi kama ifuatavyo:

## 5.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Vipimo na Viwango (Metrology Complex)

Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Vipimo na Viwango ni sehemu ya juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya usimamizi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha na kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kuimarisha mafunzo ya vitendo. Mradi huu unalenga kuboresha mazingira ya kujifunzia, kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu, na kuchangia upatikanaji wa wataalamu wenye ujuzi unaohitajika kwa maendeleo ya Taifa.

Mradi huu ulianza tarehe 25 Mei 2023 na unatarajiwa kukamilika Tarehe 23 Mei 2026. Aidha, Utekelezaji wa mradi umefikia Asilimia 93.

Taarifa hii inatoa muhtasari wa utekelezaji wa mradi huu, ikijumuisha hali ya maendeleo, matumizi ya fedha, na matarajio ya kukamilika kwake.

### 5.1.1 Lengo la Mradi

Mradi huu unalenga kupanua na kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi ongezeko la wanafunzi, kuimarisha mafunzo ya vitendo, na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Chuo cha Elimu ya Biashara.

### 5.1.2 Mkandarasi na Mshauri

Mkandarasi wa mradi huu ni LI JUN DEVELOPMENT CONSTRUCTION CO. LTD. Kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza kwa mkataba wenye thamani ya TZS. 10,398,228,771.45 ikiwa na VAT na Mshauri Mwelekezi Bureau for Industrial Cooperation (BICO) Kwa ajili ya usanifu na usimamizi wa mradi kwa mkataba wenye thamani ya TZS. 215,235,000 ikiwa na VAT.

### 5.1.3 Bajeti ya Mradi

Bajeti ya mradi huu kwa awamu ya Kwanza (ujenzi) ni **TZS 10,398,228,771.45** na awamu ya pili (makadirio) ni **TZS 16,000,000,000.00** Jumla ya gharama za mradi ni **TZS 26,398,228,771.45** kwa awamu zote mbili pamoja na gharama za mshauri elekezi. Awamu ya pili ya mradi huu inategemewa kuanza mwaka huu wa fedha, 2025 / 2026. Chuo kiko katika hatua za mwisho za kupata mkopo kwa ajili ya kutekeleza awamu hii na kunnua samani na vifaa kwa ajili ya jengo.

### 5.1.4 Malipo yaliyofanyika hadi sasa

Hadi Machi 2026, tumemlipa mkandarasi malipo ya jumla ya TZS **8,887,404,157.19** bilioni. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **TZS 6,304,371,086.43**. bilioni ni kutoka vyanzo vya mapato ya ndani na **TZS 2,583,033,070.72** bilioni ni fedha za ruzuku kutoka serikalini (Jedwali Na. 4)**.**

**Jedwali Na. 4: Bajeti ya Mradi na Malipo Yaliyofanyika Hadi Sasa**

| | FEDHA ZA NDANI | | RUZUKU YA SERIKALI | |
|---|---|---|---|---|
| | ZILIZOTENGWA | ZILIZOTUMIKA | ZILIZOTENGWA | ZILIZOPATIKANA |
| **2023/2024** | 2,000,000,000.00 | 2,000,000,000.00 | 1,050,000,000.00 | 1,049,000,000.00 |
| **2024/2025** | 2,500,000,000.00 | 2,431,256,325.43 | 700,000,000.00 | 700,000,000.00 |
| **2025/2026** | 3,800,000,000.00 | 1,873,114,761.00 | 1,000,000,000.00 | 834,033,070.72 |
| **JUMLA** | **8,300,000,000.00** | **6,304,371,086.43** | **2,750,000,000.00** | **2,583,033,070.72** |

Kwa mwaka wa fedha 2025/202,6 mradi ulitengewa jumla ya **TZS 4,800,000,000**, ambapo **TZS 3,800,000,000** ni Fedha za mapato ya ndani na **TZS 1,000,000,000** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha fedha kilicholipwa mpaka sasa kwa mwaka huu ni **TZS 834,033,070.72** kutoka Serikali kuu na **TZS 1,873,114,761.00** kutoka mapato ya ndani ya Chuo.

### 5.1.5 Manufaa ya Mradi

Mradi huu ukikamilika utaongeza uwezo wa kubeba jumla ya watu **5,594** kwa mchanganuo ufuatao:

- Maabara 5 za viwango na vipimo (wanafunzi 60 kila moja)
- Karakana 5 za viwango na vipimo (wanafunzi 60 kila moja)
- Vyumba vya semina 2 (Watu 116 kila moja)
- Ukumbi mkubwa wa watu 500
- Ofisi 51 (watumishi 102)
- Kumbi za mihadhara 29 zenye uwezo wa kubeba wanafunzi **4,160**

Hivyo, mradi huu utaongeza uwezo wa udahili, kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuimarisha ubora wa elimu.

| Mwonekano Jengo litakapokamilika | Monekano kwa sasa |
| --- | --- |
|   |  |

Umaliziwaji wa jengo hili kwa awamu ya pili utafanyika kupitia mkopo wa benki TZS Bilioni 20. Kiasi cha mkopo huu (TZS bilioni 16) kitatumika kumalizia jengo na kiasi kilichobaki (TZS Bilioni 4) kitatumika kununua samani na vifaa vya jengo. Chuo kipo katika hatua za mwisho za upatikanaji wa mkopo na ununuzi wa mkandarasi utaanza robo ya nne ya mwaka huu 2025/2026.

### 5.2 Ujenzi wa Ukumbi wa mikutano – Mwanza

Ndani ya miezi sita ya kwaka huu wa fedha, chuo kimekamilisha usanifu wa ukumbi mkubwa wa mikutano katika kampasi ya mwanza. Baada ya hapa hatua za awali za kumpata mkandarasi wa ujenzi zimekamilika na chuo kinatarajia kuanza ujenzi ndani ya mwaka huu wa fedha 2025/2026. Ukumbi huu unatarajia kuwa na uwezo wa kuchukua watu **600** kwa wakati mmoja na utajengwa kwa kutumia fedha za ndani. Mradi huu unategemea kugharimu shilingi za kitanzania **bilioni 2.49** na utasimamiwa na mshauri kwa gharama ya **TZS milioni 120.** Mkataba wa ujenzi huu utachukua kipindi cha miaka miwili. (16/03/26 – 15/03/28).

| Ukumbi wa Mikutano Mwanza |
| --- |
|  |

## 5.3 Ujenzi wa Kumbi za Mihadhara – Kampasi ya Mbeya

Katika kipindi hiki chuo kimekamilisha usanifu wa majengo ya madarasa na kumbi za mihadhara katika kampasi ya mbeya. Kazi ya usanifu pamoja na usimamizi iligharimu shilingi za kitanzania **milioni 94**. Hatua za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi tayari zimeanza. Sehemu ya ujenzi wa majengo haya ambayo ni kumbi za mihadhara tatu inategemea kuanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha 2025/2026. Kumbi hizi tatu zinategemewa kugharimu takribani shilingi **bilioni moja (1)** ambazo zitatoka katika vyanzo vya ndani. Ujenzi utaanza mara baada ya mkandarasi kupatikana kwenye robo ya nne ya mwaka huu wa fedha na utachukua kipindi cha **miezi tisa** kukamilika. Kumbi nyingine tatu zilizobakia zitajengwa kwaka ujao (2026/2027) wa fedha.  Jengo lililobakia la ghorofa nne (G + 3), litajengwa miaka ijayo ya fedha kadiri ya uwezo wa kifedha wa chuo utakavyoruhusu. Majengo yote yatakuwa na uwezo wa kuhudumia watu **3600** kwa mara moja.

| **Jengo la Kumbi za Mikutano** | **Jengo la Ofisi na Madarasa** |
|---|---|
|  |  |

## 5.4 Ujenzi wa Kampasi Mpya ya Kilimajaro

Katika kipindi hiki, Chuo cha elimu ya Biashara kimefanikiwa kupata hati ya ardhi yake iloyoko katika kijiji cha Shirinjoro wilaya ya Hai Mkoa wa Kilimanjaro. Eneo hilo lina ukubwa wa **ekari 15.64.** Kwa sasa chuo kimempata mkandarasi kwa ajili ya kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan) kwa ajili ya matumizi bora ya eneo na kusanifu majengo matatu ambayo ni:- Jengo la hoteli kwaajili ya kujifunzia, jengo la bweni la wanafunzi na Jengo la taaluma na utawala. Mradi huu wa kutengeneza mpango kabambe na kusanifu majengo umeanza tarehe **29/12/2025** na unategemea kukamilika **09/04/2026.** Tayari mkandarasi yuko eneo la kazi. Katika hatua hii ya kutengeneza mpango kabambe na kusanifu majengo ya awali yenye uwezo wa kuhudumia watu **315** kwa wakati mmoja kwa gharama ya **TZS Milioni 174**. Aidha andiko kwaajili ya fedha za mradi wa Higher Education for Economic Tatansformation (HEET) ambazo zitatumika kwa ujenzi limekamilika na limewasilishwa wizara ya elimu kwaajili ya hatua za mwisho. Chuo kinategemea kutumia **TZS Bilioni 17.6** katika mradi huu. Fedha hizi zinatarajia kupatikana mwezi wa tatu mwaka huu.

## 5.5 Usanifu wa Majengo katika kampasi ya Dodoma eneo la Nzuguni

Katika nusu ya kwanza ya mwaka huu wa fedha chuo kimekamilisha usanifu wa majengo ya awali ya kampasi ya dodoma katika eneo la nzuguni. Majengo haya yanajumuisha jengo la utawala na taaluma la ghorofa nne (G + 3) na jengo la huduma za wanafunzi la ghorofa mbili (G + 1). Kazi ya usanifu iligharimu shilingi **milioni 130** na imekamilika kwa asilimia 100. Ujenzi wa jengo moja la utawala na taaluma la ghorofa nne (G + 3) unatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha 2026/2027. Jengo hili linategemewa kugharimu shilingi za kitanzania **bilioni 12.15** na litajengwa kwa awamu kupitia fedha za ndani na fedha za maendeleo kutoka serikalini. Jengo hili litakuwa na uwezo wa kuhudumia watu **3,900** kwa wakati mmoja. Jengo jingine litajengwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**Mwonekano wa Majengo Mawili Yakikamilika**



### 5.6 Mradi wa Mabweni Dar es Salaam kwa Ubia na Sekta Binafsi (PPP)

Kwa sasa Chuo kina uwezo wa kutoa malazi kwa wanafunzi takribani **856 (3.4%)** tu katika kampasi zote nne, ikilinganishwa na wanafunzi **24,957** kwa mwaka 2025/2026 wanaohitaji huduma hiyo. Katika kutatua changamoto hii, Chuo kinakwenda kutekeleza ujenzi wa mabweni ya wanafunzi kupitia ubia kati ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Hii itasaidia kuongeza nafasi za malazi na kuboresha ustawi wa wanafunzi. Mradi wa PPP hostels kwa Kampasi ya Dar es salaam wenye thamani ya **TZS 35 bilioni,** ambao utakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi **3,600** upo katika hatua ya ununuzi kupata mwekezaji mwezi huu wa tatu mwishoni.

**Mwonekano wa Majengo Pacha ya Mabweni Kampasi ya Dar es salaam**



## 6.0 Umiliki wa Ardhi kwa ajili ya Upanuzi wa Chuo

Chuo kinamiliki ardhi katika maeneo mbalimbali kama inavyoonekana katika jedwali namba 5, linaloonesha eneo ukubwa na hali ya ardhi hizo.

**Jedwali Na. 5: Umiliki wa Ardhi**

| KANDA | WILAYA / MKOA | UKUBWA | HALI YA SASA |
|---|---|---|---|
| Kaskazini | Moshi - Kilimanjaro | Hekari 15.5 | Utengenezaji wa mpango kabambe na usanifu wa majengo unaendelea |
| Nyanda za juu kusini | Kilolo Iringa | Hekari 50 | Hati imepatikana |
| | Mufindi - Iringa | Hekari 50 | Hati inafuatiliwa |
| Kusini | Kikwetu - Lindi | Hekari 50 | Hati imepatikana |
| Zanzibar | Chwaka - Zanzibar | Ekari 2.5 | Hati imepatikana |

Baada ya kupata hati za umiliki, chuo kimeshafanya upembuzi yakinifu (Feasibility study) kwa maeneo ya Kilimanjaro, Kilolo, Mufindi na Zanzibar. Kitafanya pia upembuzi yakinifu kwa eneo lililobaki la Lindi. Chuo kitaendeleza maeneo haya kulingana na mpango wa upanuzi wa Chuo (*College Physical Geographical Expansion Plan*) uliopitishwa na Bodi ya Uongozi wa Chuo Aprili 2024 na kwa kadiri fedha zitakavyopatikana.

## 7.0 Mapato na Matumizi ya Chuo kwa Miaka Mitano

### 7.1 Mapato

Kwa kipindi cha miaka mitano, mapato ya CBE yameongezeka kutoka **TZS 26.90 bilioni** mwaka 2020/21 hadi **TZS 42.90 bilioni** mwaka 2024/25, ikionyesha ukuaji thabiti wa kifedha (Jedwali Na. 6). Sehemu kubwa ya mapato inatokana na **mapato ya ndani**, hasa ada za wanafunzi, kutoka **TZS 15.90 bilioni** mwaka 2020/21 hadi **TZS 28.15 bilioni** mwaka 2024/25, huku **Serikali ikichangia TZS 10.99 bilioni hadi TZS 14.75 bilioni** kupitia ruzuku, ikiwemo mishahara na fedha za maendeleo. Mwelekeo huu unaonyesha CBE inaendelea kuimarisha uwezo wake wa kifedha kutoka vyanzo vya ndani sambamba na

kuendeleza msaada wa Serikali katika kuendesha na kuboresha shughuli za kitaaluma na kiutawala.

**Jedwali Na 6: Mapato ya Chuo kwa Miaka Mitano**

| Mwaka wa Fedha | Fedha kutoka Serikalini (TZS) | Mapato ya Ndani (TZS) | Jumla ya Mapato (TZS) |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 10,997,191,591 | 15,949,881,065 | 26,947,072,655 |
| 2021/2022 | 12,078,755,647 | 15,790,862,952 | 27,869,618,599 |
| 2022/2023 | 12,896,505,522 | 21,903,685,756 | 34,800,191,278 |
| 2023/2024 | 14,706,750,138 | 23,530,629,879 | 38,237,380,017 |
| 2024/2025 | 14,749,445,690 | 28,158,430,631 | 42,907,876,321 |

### 6.1 Matumizi

Kwa kipindi cha miaka mitano, jumla ya matumizi ya CBE imeongezeka kutoka **TZS 25.68 bilioni** mwaka 2020/21 hadi **TZS 42.78 bilioni** mwaka 2024/25 (Jedwali Na. 7). Sehemu kubwa zaidi ni mishahara na matumizi ya uendeshaji, ikionyesha ongezeko la wafanyakazi na gharama za kila siku, huku miradi ya maendeleo na matumizi mengine ikitekelezwa kwa kiwango kidogo. Mwenendo huu unaonyesha chuo kinatumia mapato yake kikamilifu, kikizingatia ufanisi wa kiutawala na utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

**Jedwali Na 7: Matumizi ya Chuo kwa Miaka Mitano**

| Mwaka wa Fedha | Mishahara (TZS) | Uendeshaji (OC) (TZS) | Miradi ya Maendeleo (TZS) | Matumizi Mengineyo (TZS) | Jumla ya Matumizi (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 10,917,462,386 | 7,648,548,226 | 2,767,533,678 | 4,349,974,291 | 25,683,518,581 |
| 2021/2022 | 11,474,405,585 | 8,192,879,914 | 4,302,676,449 | 4,374,225,076 | 28,344,187,024 |
| 2022/2023 | 12,673,488,323 | 15,958,923,131 | 3,115,128,726 | 2,497,092,030 | 34,244,632,210 |
| 2023/2024 | 14,706,750,137 | 18,198,471,322 | 5,159,148,793 | 1,448,132,997 | 39,512,503,249 |
| 2024/2025 | 14,749,445,690 | 21,678,490,537 | 4,253,451,426 | 2,107,820,793 | 42,789,208,446 |

### 6.2 Ulinganisho wa Mapato na Matumizi

Kwa miaka mitano, mwenendo wa kifedha wa CBE umeonyesha mwelekeo mzuri na udhibiti wa matumizi. Baada ya tofauti hasi kidogo mwaka 2021/22 na 2023/24, kuanzia 2024/25 mapato yamezidi matumizi, ikionyesha udhibiti thabiti na usawa wa kifedha (Jedwali Na. 8).

**Jedwali Na 8: Ulinganisho wa Mapato na Matumizi**

| Mwaka wa Fedha | Jumla ya Mapato (TZS) | Jumla ya Matumizi (TZS) | Tofauti (Mapato – Matumizi) |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 26,947,072,655 | 25,683,518,581 | 1,263,554,074 |
| 2021/2022 | 27,869,618,599 | 28,344,187,024 | (474,568,425) |
| 2022/2023 | 34,800,191,278 | 34,244,632,210 | 555,559,068 |
| 2023/2024 | 38,237,380,017 | 39,512,503,249 | (1,275,123,232) |
| 2024/2025 | 42,907,876,321 | 42,789,208,446 | 118,667,875 |

Tofauti chanya kwa mwaka 2020/2021 ilitokana na malipo ya mwaka 1920/2020 yaliyovuka mwaka na kulipwa mwaka uliofuata kutokana na athari za UVIKO 19. Miaka iliyofuata 2021/2022 na 2023/2024 ilionekana kuwa na tofauti hasi (Deficit) kutokana na kukua kwa matumizi ya chuo yaliyotokana na kuongezeka kwa watumishi na shughuli za maendeleo (Ujenzi wa Kampasi ya Mbeya na ujenzi wa jengo la Legal metrology Dae es Salaam). Miaka iliyofuata baada ya hapo, chuo kiliendelea kuwa na tofauti chanya (Surplus) kutokana na usimamizi mzuri wa mapato na matumizi.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Chuo kimeendelea kuboresha usimamizi wa fedha kwa kuzingatia vyanzo vya mapato ya ndani na fedha kutoka Serikali. Muhtasari wa bajeti na utekelezaji wa nusu mwaka (Julai–Desemba 2025) umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 9

**Jedwali Na. 9: Utekelezaji wa Bajeti Nusu Mwaka 2025/2026 (Julai – Desemba 2025)**

| BAJETI | MAPATO | MATUMIZI | ZIADA |
|---|---|---|---|
| 58,800,000,000 | 26,571,000,000 (44.6%) | 24,040,000,000 | 2,531,000,000 |

Kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Desemba 2025), chuo kimeweza kukusanya **asilimia 44.6** ya bajeti yake. Baada ya matumizi, kimesalia na ziada ya bajeti ya **TZS bilioni 2.5**,

kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 9. Hali hii inaonesha ustahimilivu mzuri wa kifedha kwa kipindi husik

## 8.0 Hitimisho

Kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana katika taaluma, utafiti, ushauri wa kitaalamu, uendelezaji wa miundombinu na usimamizi thabiti wa rasilimali fedha, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kinaendelea kujijengea msingi imara wa ukuaji endelevu na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara nchini. Pamoja na changamoto zilizopo, mikakati iliyowekwa inaonesha utayari wa chuo kuimarisha ubora, kupanua fursa za ajira kwa vijana na kuongeza mapato ya ndani kwa ufanisi zaidi. Kwa msingi huo, CBE itaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara na wadau mbalimbali ili kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kuchangia kikamilifu katika utekelezaji wa malengo ya kitaifa.

Naomba Kuwasilisha.

**JUDITH SALVIO KAPINGA (MB)**

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA